# Udhibiti wa magugu katika mfumo wa uzalishaji wa Kikaboni

Kwa kuwa ni jambo kuu katika kilimo, rutuba ya udongo huamua ubora na wingi wa mazao yanayokuzwa katika kipande fulani cha ardhi.
Wakati usimamizi wa magugu ukiendelea kuwa changamoto inayowakabili wakulima wa kilimo-hai, ongezeko la mbegu za magugu hupunguza mavuno, na vipengele vikuu vya udhibiti wa magugu haya ni mazao, kutumia bomba la umwagiliaji na kisha kulifanya likawa bomba la kutonesha kati ya siku 10 hadi 14.

## Usimamizi wa magugu

Kwa vile muda ni jambo muhimu katika udhibiti wa magugu, shamba humwagiliwa maji wakati wa kupanda. Hata hivyo, hakikisha kwamba 1 inchi ya udongo imepenywa maji. Siku 4 baadaye, mwagilia huku ukihakikisha kwamba 1/2 inchi ya udongo imepenywa maji. Siku ya 7 baadaye, mwagilia huku ukihakikisha kwamba 1/2 inchi ya udongo imepenywa maji. Siku ya 11, udongo utakuwa tayari kulimwa.
Vile vile, tumia maji ya kutosha kwa ukuaji wa mimea na uhakikishe unalima udongo ipaswavyo, palilia mapema iwezekanavyo katika siku 10-14 kwa kutumia mbinu bora za palizi ili kuua magugu. Baada ya kupalilia magugu yaliyo juu ya kitalu, tumia jembe maalum la trekra kulima udongo na kuondoa magugu kati ya safu za vitalu.
Acha nafasi ya inchi 72 kutoka katikati ya tairi moja ya trekta hadi tairi nyingine. Weka jembe 3 kwa trekta kwa umbali wa inchi 36 kutoka moja hadi lingine.
Katika trekta hiyo, vifaa muhimu vya kulima ni jembe, patasi ili kuvunja mabonge ya udongo, na kisu cha pembeni ambacho hufanya kazi kando ya vitalu. Jembe linapaswa kuwekwa nyuma ya  matairi ya trekta kwa uendeshaji mzuri.
Hatimaye wakati wa kuleta trekta shambani, kumbuka muundo wa vitalu, weka mirija ya kutonesha kwenye vitalu, na mwagilia maji ili kuotesha magugu zaidi.